UTENDI WA MWANAKUPONA

1. Negema wangu binti
   Mchachefu wa sanati
   Upulike wasiati
   Asa ukazingatia

2. Maradhi yamenishika,
   Hatta yametimu mwaka
   Sikupata kutamka
   Neno lema kukwambia

3. Ndoo mbee ujilisi
   Na wino na qaratasi
   Moyoni nina hadithi
   Nimependa kukwambia

4. Ukisa kutaqarabu
   Bismillahi kutubu
   Umsalie Habibu
   Na sahabaze pamoya

5. Ukisa kulitangaza
   Ina la Mola Muweza
   Basi tuombe majaza
   Mola tatuwafiqia

6. Mwanaadamu si kitu
   Na ulimwengu si wetu
   Walau hakuna mtu
   Ambao atasalia

7. Mwanangu twaa waadhi
   Pamoya na yangu radhi,
   Mngu atakuhifadhi,
   Akuepushe na baa

8. Twaa nikupe hirizi
   Uifungeto kwa uzi
   Uipe na taazizi
   Upate kuyangalia

9. Nikutungie kindani
   Cha lulu marijani
   Nikuvike mke shani
   Shingoni kikizagaa

10. Penda nikupe kifungo
    Kizuri kisicho ongo
    Uvae katika shingo
    Utaona manufaa

11. Yangu utakaposhika
    Mwanangu hutosumbuka
    Duniani utavuka
    Na akhira utakia

12. La kwanda kamata dini
    Faradhi usiikhini
    Na sunna ikimkini
    Ni wajibu kuitia

13. Pili uwe na adabu
    Na ulimi w athawabu
    Uwe mtu mahabubu
    Kula utakapoingia

14. La tatu uwe sadiqi
    Wambiwalo ulithiqi
    Mtu asoshika haqi
    Sandamane naye ndia

15. Tena mwanangu idhili
    Mbee za maqabaili
    Uwaonapo mahali
    Angusa kuwenukia

16. Wangiapo wenukie
    Na moyo ufurahie
    Kisa uwapeke mbee
    Watakapokwenda ndia

17. Ifanye mteshiteshi
    Kwa maneno yasoghashi
    Wala sifanye ubishi

UTENDI WA MWANAKUPONA

Watu wakakutukia

18. Nena nao kwa mzaha
    Yaweteao furaha
    Iwapi ya ikraha
    Kheri kuinyamalia

19. Wala situkue dhana
    Kwa mambo usoyaona
    Na kwamba na kunong'ona
    Tahadhari nakwambia

20. Sitangane na watumwa
    Ilia mwida wa khuduma
    Watakuvutia tama
    La buda nimekwambia

21. Sandamane na wainga
    Wasyua kuitunga
    Ziumbe wasio tanga
    Wala kuwaqurubia

22. Mama pulika maneno
    Kiumbe ni radhi tano
    Ndipo apate usono
    Wa akhera na dunia

23. Nda Mngu na mtumewe
    Baba na mama wayuwe
    Na ya tano nda mumewe
    Mno imekaririwa

24. Naawe radhu mumeo
    Siku zote mkaao
    Siku mukhitariwao
    Awe radhi mekuwea

25. Na afapo wewe mbee
    Radhi yake izengee
    Wende uitukuzie
    Ndipo upatapo ndia

26. Siku ufufuliwao
    Nadhari ni ya mumeo
    Taulizwa atakao
    Ndilo takalotendewa

27. Kipenda wende peponi
    Utakwenda dalhini
    Kinena wende motoni
    Huna bundi utatiwa

28. Keti naye kwa adabu
    Usimtie ghadhabu
    Akinena simjibu
    Itahidi kunyamaa

29. Enda naye kwa imani
    Atakalo simkhini
    We naye sikindaneni
    Ukindani huumia

30. Kitoka agana naye
    Kingie mkongowee
    Kisa umtengezee
    Mahala pa kupumua

31. Kilala siikukuse
    Mwegeme umpapase
    Na upepo asikose
    Mtu wa kumpepea

32. Kivikia simwondoe
    Wala sinene kwa yowe
    Keti papo siinue
    Chamka kakuzengea

33. Chamka siimuhuli
    Mwandikie maakuli
    Na kumtunda muili
    Kumsinga na kumwoa

UTENDI WA MWANAKUPONA

34. Mnyoe mpatilize
Sharafa umtengeze
Na udi umfukize
Bukuata wa ashia

35. Mtunde kama kijana
Asiyojua kunena
Kitu changalie sana
Kitokacho na kungia

36. Mpumbaze apumbae
Amriye sikatae
Maovu kieta yeye
Mngu atakulipia

37. Mwanangu siwe mkoo
Tenda kama uonao
Kupea na kosha choo
Sidharau mara moya

38. Na kowa na kuisinga
Na nyee zako kufunga
Na smini kutunga
Na firashani kutia

39. Nawe ipambe libasi
Ukae kama arusi
Maguu tia kugesi
Na mikononi makoa

40. Na kidani na kifungo
Sitoe katika shingo
Muili siwate mwingo
Kwa marashi na daiia

41. Pete sikose zandani
Hina sikome nyaani
wanda sitoe matoni
Na nshini kuitia

42. Nyumba yako i nadhifu
Mumeo umsharifu
Wakutanapo sufufu
Msifu ns kumiaya

43. Muyuwe alipendalo
Nawe ufuate lilo
Yambo limtukialo
Siwe mwenye kumwetea

44. Na ukitaka kutoka
Sharuti rukhusa taka
Wonapo meudhika
Rudi na kuikalia

45. Fuata idhini yake
Awe radhi kwa yaqini
Wala sikae ndiani
Saa yane ikasia

46. Wala sinene ndiani
Sifiinue shiraani
Mato angalia tini
Na uso utie haya

47. Rejea upesi kwako
Ukae na mume wako
Utengeze matandiko
Mupate kuilalia

48. Mume wako mtukuze
Sifa zake zieneze
Wala simsharutiye
Asichoweza kutoa

49. Akupacho mpokee
Na moyo ufurahie
Asolitenda kwa yeye
Huna haja kumwambia

50. Uonapo uso wake
Funua meno uteke

UTENDI WA MWANAKUPONA

Akwambialo lishike
Ilia kuasi Jalia

51. Mama sinue ulimi
Nioleza wako umi
Nalioa nyaka kumi
Tusitete siku moya

52. Alinioa babako
Kwa furaha na ziteko
Tusondoleane mbeko
Siku zote twaiokaa

53. Siku moya tusitete
Ovu langu asipate
Na lake nisilikute
Hatta akakhitariwa

54. Yalipokuya faradhi
Kanikariria radhi
Kashukuru kafawidhi
Moyo wangu katoshea

55. Tangu hapo hatta yeo
Siyanyamaa kilio
Nikumbukapo pumbao
Na wingi wa mazoea

56. Watu wakipulikana
Milele hukumbukana
Ilia wenye kushindana
Daima huiyutia.

57. Mausio ya mvuli
Allah Allah yaamili
Na nduguzo na ahali
Wapende nakuusia

58. Uwaonapo swahibu
Ambao wakunaswibu
Wakwambiapo qaribu
Angusa kuqurubia

59. Na wachandika chakula
Uchambiwa nawe nia wala
Siweke muhula
Nyumanyuma kurejea

60. Wala sifanye kiburi
Nia hata ushakiri
Usiyakuta siqiri
Ukamba ni kondolewa

61. Watu wote waumini
Kwako na wawe wendani
Sipende masalatini
Washinde ukiwepua

62. Sipende wenye jamali
Na utukufu wa mali
Fuqara ukamdhili
Cheo ukamvundia

63. Akupendao mpende
Akuizao mwenende
Kwa zema mvundevunde
Laana akiridhia

64. Na ayaapo muhitaji
Mama kwako simuhuji
Kwa uwezalo mbuji
Angusa kumtendea

65. Mama haya yasikize
Tafadhali sinipuze
Utaona nafuuze
Za akhera na dunia

66. Tamati maneno yangu
Kukuusia mwanangu
Sasa tamuomba Mngu
Anipokelee dua

UTENDI WA MWANAKUPONA

67. Kwani yote ninenao
Mwanaadamu ni puo
Mola ndiye awezao
Kupoteza na kongoa

68. Nakuombawe Manani
Umtilie auni
Ninenayo ulimini
Na yote nisoyatoa

69. Yote nimezoyanena
Rabbi taqabali minna
Na yasalieo tena
Rabbi Mola nitendea

70. Niwekea wangu wana
Na umbu iangu mnuna
Yakue yao maina
Yanee majimbo pia

71. Rabbi waweke nduzangu
Na wana wa ndugu zangu
Wende na ulimwengu
Kwa jamala na sitawa

72. Na jamii islamu
Mola wangu warehemu
Matakwa yao yatimu
Na nyoyo kufurahia

73. Ya Allahu wangu wana
Nimekupa ni amana
Watunde Mola Rabana
Siwate kuwangalia

74. Nimekupa duniani
Watunde uwakhizini
Unipe kesho peponi
Mbee za Tumwa Nabia

75. Wangalie kwa huruma
Waongoze ndia njema
Uwepulie na tama
Za akhira na dunia

76. Kukuombawe sikome
Wala sifumbi ulimi
Ya Mufarrija ‘1Hammi
Nikomeshee ushia

77. Nisimeme muhitaji
Mjao nakutaraji
Ajili bi’lfaraji
Ya afua na afia

78. Nondolea ndwee mbovu
Yaloningia kwa nguvu
Dhambi zangu na maovu
Ya Rabbi nighufma

79. Kwetu yangawa mazito
Kwako wewe ni matoto
Nepulia uvukuto
Uepuke mara moya

80. Nakuombawe Latifa
Unondolee makhafa
Kwa yaumu ‘1Arafa
Na idi ya udhia

81. Kwa siku hizi tukufu
Za kuhiji na kutufu
Niafu Rabbi niafu
Unishushize afua

82. Ya Ailahu ya Ailahu
Ya Rabbahu ya Rabbahu
Ya Gjayata Raghbatahu
Niyika hukwamkuwa

83. Nakuombawe Rabbana

Bi amaila 'Ihusna
Tisia wa tisiina
Mia kungua moya

84. Nipulishie walimu
Wakinena yafahamu
Dua hini Islamu
Akiomba hujibiwa

85. Nami mjao dhaifu
Mwenye nyingi taklifu
Nakuomba takhfifu
Rabbi nitakhafifia

86. Nakuomba taisiri
Mambo nisoyaqadiri
Unengeshe kulla kheri
Shari ukinepulia

87. Ya Rabbi nitimiliza
Mambo nisiyoyaweza
Wala moyoni kuwaza
Kwamba yatasikitia

88. Rabbi unifurahishe
Mambo mema unengeshe
Maovu uyagurishe
Tusikutane pamoya

89. Uniweke duniani
Miongo ya wahusuni
Nifapo nende peponi
Makao ya hafidhiwa

90. Tungiie utungo hunu
Kwa zehemu na zitumu
Kwa qadha yako Dayyanu
Na hukumuzo Jalia

91. Tungilie nili saqimu
Moyo usina fahamu
Usomeni Islamu
Mukiogozana ndia

92. Na sababu ya kutunga
Si shairi si malenga
Nina kijana muinga
Napenda kumuusia

93. Napenda kumkabihi
Laala katanabahi
Kamfuata illahi
Pamwe na wake rijaa

94. Somani nyue huramu
Maana muyafahamu
Musitukue laumu
Mbee za Mola Jalia

95. Somani mite ya nganu
Mutii waume wenu
Musipatwe na zitunu
Za akhera na dunia

96. Mwenye kutii mvuli
Ndake jaha na jamali
Kula endapo mahali
Hutangaa yake ndia

97. Mwenye kutunga nudhumu
Ni gharibu mwenye hamu
Na ubora wa ithimu
Rabbi tamghufiria

98. Ina lake mufahamu
Ni mtaraji Karimu
Mwana Kupona Mshamu
Pate alikozaliwa

99. Tarikhiye kwa yaqini
Ni alifu wa miyateni
Khamsa na sabiini

Hizi zote hijiria

100. Na baitize idadi
Ni miati maadudi
Na mbili za mazidadi
Ndizo zimezozidia

101. Mola tatusahilia
Kwa Baraka za Nabia
Na masahaba pamoya
Dini waliotetea

102. Nahimidia kisalia
Kwa tume wetu nabia
Ali zake na dhuria
Itwenee sote pia."